Sen. Sakaja: Madam Deputy Speaker, responses were given to both. I think we just need to check with the secretariat, because a response was given. On the issue of the emergency fund, a response was given to the Committee on the COVID-19 situation in

Kenya, which I was chairing at that time. That response has been shared. If the Senator is not satisfied with that response, we can reopen it at any time.

On the issue of pensions, I will check with my secretariat, but I believe that we also dealt with that. There was a response. I will just check with her right now and will respond before the end of this Sitting.

In fact, I am happy that after the two Petitions that I have laid, my Committee is the only one that has no pending Petition. I am very proud of that. I am keen on this one and need to find out.

The Deputy Speaker (Sen. Prof.) Kamar: Sen. Were, we have problem with our Standing Orders because they do not ask the Committee to refer back to the Petitioners or Members who were asking. It is only courteous that they receive a copy of the report. The secretariat must also take note of that.

Do you still want to pursue something?

Sen. Were: Yes. I want to make a clarification. A response was given on the Statement on the emergency fund within trade unions months ago. It was unsatisfactory and I communicated this. Sen. Sakaja said that since he is also the Chair of the Committee on Labour and Social Welfare, it would be redirected to his Committee and he would deal with it. However, I have not received a response.

The Deputy Speaker (Sen. Prof.) Kamar: Since you had already communicated, I would like to encourage that you discuss further and see that you bring it to a conclusion, Sen. Sakaja.

We have two more Statements. We are way past our time for Statements. We want a Statement to be read by the Committee on Health under Standing Order 47 (1). Sen. Seneta will read a Statement regarding the commemoration of the World AIDS Day in the context of COVID-19, and thereafter, I will have the Majority Whip to read a Statement on the future programme.

Sen. Seneta.

Sen. Seneta: Thank you, Madam Deputy Speaker. Before I read the Statement, on behalf of the Chair, I thank Sen. Sakaja and the rest of the Members who appreciated our efforts as the Committee. I assure them that we will work hard to help in matters health.

Thank you so much for the trust.

COMMEMORATION OF WORLD AIDS DAY IN
THE CONTEXT OF THE COVID-19 PANDEMIC

Sen. Seneta: I rise pursuant to Standing Order 47(1) to make a Statement on an issue of general topical concern, namely, the commemoration of World AIDS Day in the context of the COVID-19 pandemic.

Madam Deputy Speaker, the World AIDS Day was established in 1988 as an international day to raise awareness on the Human Immunodeficiency Virus (HIV) pandemic, and is marked on 1st December every year. The event provides an opportunity to unite the globe to stop new HIV infections, support those infected and affected by HIV, and remember those who have lost their lives due to AIDS.

This year's World AIDS Day is being commemorated today, Tuesday, 1st December, 2020. Every year, the National AIDS Control Council (NACC) engages the

national Government and county governments, and mobilizes partners and stakeholders in all 47 counties to participate in the event.

The global theme for this year's campaign as per the joint United Nations Programme on AIDS (UNAIDS) is "Global Solidarity; Shared Responsibility". The theme underscores the significance of individuals, countries and the global community uniting in taking responsibility to address HIV and AIDS amidst the growing list of challenges that the World is facing today, including the COVID-19 pandemic.

[The Deputy Speaker (Sen. (Prof.) Kamar left the Chair]

[The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura) in the Chair]

Mr. Temporary Speaker, Sir, Kenya has adopted the 'Komesha HIV & COVID 19 #Tuwajibike' as the national theme. This is in line with the efforts of the Government towards preventing the spread of HIV and COVID-19. The aim is to call out for the ending of the spread of HIV and COVID-19 through citizens and Government partnership and co-operation.

Since the first case of HIV was officially recorded in Kenya in 1984, approximately 1.9 million people have lost their lives in Kenya as a result of HIV/AIDS related complications. By the end of 2019, the HIV prevalence rate stood at 4.5 per cent with approximately 1.5 million people living with HIV. At the same time, the prevalence of HIV is higher among women who have a prevalence rate of 5.8 per cent compared to the 3.1 per cent among men.

In 2019, there was an estimated 41,416 new infections and 20,997 HIV/AIDS related deaths across all ages; a decrease from the 101,560 new infections and 58,465 deaths in 2013 respectively. Despite the positive trajectory in the HIV and AIDS response---

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Samahani Sen. Seneta, nakuomba uzungumze kwa mukhtasari tafadhali.

Sen. Seneta: Mr. Temporary Speaker, Sir, I will try.

Despite this positive trajectory in the HIV and AIDS response registered in Kenya, various social, legal and policy challenges continue to impede effective response to HIV, notable being Stigma, discrimination and limited access to justice for the affected and infected. This is despite the enactment of the HIV and AIDS Prevention and Control Act (HAPCA) 2006 to ensure prohibition of HIV-related stigma and discrimination. In addition, the country established and operationalized the HIV and AIDS Tribunal to increase access to justice against all forms of HIV stigma and discrimination.

Mr. Temporary Speaker Sir, the emergence of COVID-19 pandemic, however, has led to far-reaching ramifications on all sectors of national and global economies. The COVID-19 pandemic has had direct negative consequences on the fight against HIV risking, eroding the gains made thus far, especially on the Global target of 90-90-90.

Both COVID-19 and HIV control require the participation of citizenry and governments to control the two pandemics. The Government of Kenya, therefore, has put in place a number of restrictions to control the spread of COVID-19, including but not limited to the daily curfews and restriction in the number of participants in public

gatherings. It is against this background that the World AIDS Day 2020 will be commemorated under special circumstances.

Mr. Temporary Speaker, Sir, we have seen how the COVID-19 crisis has exacerbated the challenges faced by people living with HIV, women and girls and key populations, including in accessing life-saving health care, and how the crisis has widened the social and economic inequalities that increase the vulnerability of marginalized groups to HIV. However, this crisis has also been a wake-up call, an opportunity to do things differently, better and together. In many respects, the defeat of AIDS as a public health threat depends on how the world responds to COVID-19.

Mr. Temporary Speaker, Sir, the COVID-19 has also shown how political will can bring about change. We have seen governments putting in place extraordinary policy measures and financial resources to save lives and protect livelihoods. We have seen collaboration between countries to ensure continuity of HIV treatment and we have seen countries rallying behind the international call to make a COVID-19 vaccine a People's Vaccine, available to all equitably. As we enter the last decade of action to end AIDS as a public health threat by 2030, we need the political will to reach our goal. It can be done!

Global solidarity and shared responsibility requires us to view global health responses, including the AIDS response, in a new way. It requires the world to come together to ensure that health is fully financed, health systems are strengthened, access to life-saving medicines, vaccines and diagnostics is ensured as a public good, human rights are respected and the rights of women and girls, and gender equality are at the centre.

The latest progress report of the Global HIV Prevention Coalition, launched on 23rd November, 2020 in Geneva, shows that despite observed declines in new HIV infections among adults in several countries, overall progress in HIV prevention efforts remains variable and is too slow to reach the 2020 targets committed to at the 2016 United Nations High-Level Meeting on Ending AIDS. This is where United Nations Member States committed to reach a worldwide HIV prevention target of fewer than 500,000 new HIV infections among adults by 2020, a 75 per cent reduction from 2010. By the end of 2019, the reduction was at just 23 per cent, with 1.7 million people becoming infected with HIV last year.

Mr. Temporary Speaker, Sir, allow me to conclude by saying that now is the moment for bold leadership for equal societies, the right to health for all and a robust and equitable global recovery. This World AIDS Day, join me in calling on counties to step up their efforts to achieve the quest for HIV and AIDS reduction. This World AIDS Day, let us demand national solidarity and shared responsibility.

I thank you.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Sasa hivi, nampa Sen. Pareno nafasi.

ACTIVITIES OF THE COMMITTEE ON NATIONAL
SECURITY, DEFENCE AND FOREIGN RELATIONS

Sen. Pareno: Mr. Temporary Speaker, Sir, I wish this statement had been done in Kiswahili; I would have read it in Kiswahili. I would like to make a Statement relating to the activities of the Standing Committee on National Security Defence and Foreign Relations.

Mr. Temporary Speaker Sir, I rise pursuant to standing Order 51 (1) (b) to make a Statement on the activities of the Standing Committee on National Security, Defence and Foreign Relations for the period commencing 1st March to 30th September, 2020.

During the period under review, the Committee held a total of 13 sittings, dealt with three Petitions, nine Statements, one Bill and one inquiry.

In respect to the Petitions, the Committee considered the following: -

(i)Petition regarding enactment of a Military Veteran Law – the Committee held a meeting with the Petitioners and resolved to enact a law to be sponsored by Sen. Pareno. A report on the matter will be laid on the Table after consideration by the Committee;

(ii)Petition regarding the Perennial Landslides and Mudslides owing to heavy rains in Nandi County - the Committee held a meeting with the Petitioner and is scheduled to hold another meeting with the Cabinet Secretary, Ministry of Lands and the National Land Commission and other stakeholders; and,

(iii)Petition on the rising insecurity cases in Laikipia County - The Committee held a meeting with the Petitioner and is scheduled to hold other meetings with other stakeholders.

In respect of Bills, the Committee considered the pre-publication scrutiny of the Kenya Citizenship and Immigration (Amendment) Bill (Senate Bills No. 12 of 2020) on Tuesday, 21st July, 2020 and recommended for its publication. The Bill has since been published and forwarded to the Committee for consideration.

In respect to the inquiry, the Committee inquired on the whereabouts of three Senators namely- Sen. (Dr.) Lelegwe, Sen. (Dr.) Langat and Sen. Malalah, as directed by the Speaker on 17th August, 2020 and laid its report in the Senate.

Mr. Temporary Speaker Sir, during the period under review, the Committee considered the following Statements: -

(1)Statement request by Sen. Mwangi, regarding unresolved murder cases in Ol-Jororok in Nyandarua County. The Committee considered the response in the presence of Sen. Mwangi and the matter was concluded.

(2)Statement request by Sen. Cherargei, Regarding Extra-Judicial Killing by Police of Kevin Kipchumba and Boniface Kiprotich in Tabolwa Village Mosop Constituency in Nandi County. The Committee considered the response by the Ministry in the presence of the Sen. Samson Cherargei who promised to supply further information on the Statement to the Committee to enable it address the Statement adequately. Owing to lack of this further information the Committee regarded the Statement as concluded.

(3)Statement request by Sen. (Dr.) Ali, regarding Police brutality on Residents of Bute and Biyamafo, in Wajir County. The Senator was given a copy of the response and was satisfied. The Committee regarded the Statement as concluded matter.

(4)Statement request by Sen. Khaniri, regarding the increased cases of insecurity in Vihiga County. The was furnished with the response and was satisfied hence the matter was concluded.

(5)There was a Statement requested by Sen. Dullo regarding torture and extra-judicial killings of residents of Isiolo County by Kenya Wildlife Service officers. The Committee invited the Director General of KWS where the Committee was presented with responses. The Senate was not satisfied with the responses and the Committee has since resolved to hold other meetings to deliberate further on the Statement.

(6) We had a Statement requested by Sen. Dullo regarding smuggling of Marijuana from Ethiopia. The Committee invited the Inspector General (IG) of Police for a meeting. The Senator who had sought the Statement requested that it be postponed. The security agencies have since sent their responses, which have since been forwarded to the Senator for further comments.

(7) We had a Statement requested by Sen. (Dr.) Milgo regarding mysterious cases of death and injuries in Bomet County. The response was forwarded to the Senator who had sought the Statement. The Committee considered the matter in the absence of the Senator and the Committee was satisfied with the response and considered the matter as concluded.

(8) There was a Statement by Sen. Omanga regarding the alleged delay in issuance of certificates of good conduct. The Committee considered the matter in the absence of Sen. Omanga and was satisfied by the response given by the Ministry and the matter was concluded.

Mr. Temporary Speaker, Sir, the Committee intends to carry out the following activities during the next quarter-

- (1) Hold a meeting with the Cabinet Secretary (CS) for Interior and Coordination of National Government to deliberate on the ravaging, abductions and disappearance of members of public occurring in various parts of the country.
- (2) Hold a meeting with CS for Lands, Environment and Natural resources and the Chairperson of the National Land Commission to deliberate on the mudslides and landslides occurring in various parts of the country and how quickly it can be mitigated by the disaster kitty.

That is all for the Committee.

I thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir.

Sen. Faki: On a point of order, Mr. Temporary Speaker, Sir.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura: Ipi Hoja ya Nidhamu?)

Sen. Faki: Mhe. Spika wa Muda, kwanza naipongeza Kamati kwa hiyo Ripoti yake, lakini masikitiko ni kwamba Kamati hii haijaangazia Taarifa yangu ambayo nilileta hapa Tarehe 24 Mwezi wa Tano mwaka huu kuhusiana na kuangushwa kwa ndege ya Kenya nchini Somalia. Ndege ile ilikuwa ya Shirika la African Express Airways ambayo ilipigwa ikiwa inatua katika uwanja mmoja nchini Somalia.

Mwezi uliopita pia nilipewa fursa kuikumbusha Kamati hii kwamba hiyo Taarifa bado haijajibiwa na kwamba tunahitaji majibu kwa haraka kwa sababu kuna ripoti inayotakikana kutayarishwa na nchi ya Somalia ambamo ndege ilianguka.

Ripoti ile itasaidia kulipwa ridhaa kwa wale waliohusika katika ajali ile ambayo marubani wawili na wasaidizi wao walipoteza maisha yao.

Ni muhimu kwamba Kamati hii ilipe Bunge hili ripoti kwa ufasaha, ni lini watazingatia mambo hayo ikizingatiwa kwamba madai ya malipo kwa familia za wale waliopoteza maisha yao baada ya mwaka mmoja kutoka tarehe ya ajali. Ajali ilitokea mwanzoni mwa Mwezi wa Tano. Kwa hivyo, imebaki takriban miezi mitano kitambo madai yao yafe.

Vile vile, hatujapata ripoti ambayo itatupa mwongozo ni nani wa kulaumiwa kuhusiana na ajali ile. Ningependa nipate ufafanuzi wa swala hilo.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura: Umejieleza vizuri sana. Ninampa nafasi Mwenyekiti, Sen. Pareno, aweze kujibu kwa sababu ya muda.

Sen. Pareno: Kwa sababu mwenzangu ametumia Lugha ya Kiswahili na pia Naibu Spika wa Muda ameendelea kwa lugha hiyo hiyo, hata mimi ninaweza kujibu haya kwa lugha ya Kiswahili.

Ni jukumu langu kama Mwanakamati wa Kamati ya Usalama Nchini kufahamisha Kamati and Mwenyekiti kwamba Taarifa ya Sen. Faki haijashughulikiwa. Nitahakikisha imeshughulikiwa na Kamati yangu.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Swala hilo limeshughulikiwa.

Sen. (Dr.) Zani, hoja yako ya nidhamu ni ipi?

Sen. (Dr.) Zani: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. If Sen. Faki had not been here, we would not have realized that there are a couple of Statements that miss out in Committees. Since he is here and has raised them, I have a feeling that the same thing might be happening in other Committees.

I suggest that moving forward, we have a way that even as we make the reports to the House, we state all the Statements that have been received and then move on to tackle those that have been tackled at the Committee. That will help us avoid a gap within the House.

Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Ningependa kuelekeza kwamba Makarani wetu watusaidie kufuatilia hizi Arifa na Kauli ndiposa zisiweze kutokomea, kwa sababu haziwezi kuwekwa rasmi katika Ripoti za Kamati.

Sasa hivi nampa nafasi, Kiranja wa Walio Wengi wa Seneti.

(Interruption of debate on Statements)

PROCEDURAL MOTION

EXTENSION OF SENATE SITTING TIME

Sen. Kang'ata: Mr. Temporary Speaker, Sir, I beg to move the following Motion:

THAT, pursuant to Standing Order No. 31 (3) (a), the Senate resolves to extend its Sitting until the conclusion of business listed as in Order No.19 in today's Order Paper.

The reasons are simple. There are two key Motions that we need to dispense with today. The first one is on the Presidential Speech to the Parliament. It needs to be concluded. There were several Senators who wanted to speak on that Motion. Therefore, we need to allow them to converse and make their point.

Mr. Temporary Speaker, Sir, after we are done with that, I will be moving a Motion that we adjourn. During that Motion, several Senators will be interested to say something and also contribute, taking into account that if that Motion is done with, we shall take a break, which will be prolonged.

I beg to ask colleagues to support this Motion, so that we give each Senator an opportune time to speak before we take the prolonged break after today.

I urge colleagues to support this Motion.

I beg to move and ask my colleague, the Chairman of the Committee on Justice, Legal Affairs and Human Rights in the Senate, Sen. Omogeni, to second.

Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir.

Sen. Omogeni: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. I second the Motion that has been put forth by the Senator for Murang'a, who is the Senate Majority Whip.

It is true that we still have some business that is pending and it is only fair that we give Senators in the House ample opportunity to make contributions to the Adjournment Motion.

I second.

(Question proposed)

Sen. Kang'ata: Mr. Temporary Speaker, Sir, if I heard you right, I think the way you have crafted your prayer, it appears like it does not rhyme with my actual Motion. This is because if I have heard the Chair right, he seems to suggest that it is after we have dispensed with all business appearing on the Order Paper, whereas mine is specific to Order No.19.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Tafadhali Kiranja wa Walio Wengi, tutaweza kumaliza orodha yote hii ya Hoja mpaka Hoja Nambari 19. Kwa hivyo, tunazungumza ipasavyo.

Hoja ya nidhamu, Sen. Sakaja.

Sen. Sakaja: Bw. Spika wa Muda, ukiangalia Kanuni zetu za Kudumu, Kipengele cha 93 kinasema kwamba Mbunge yeyote anaweza kuibua Hoja ya nidhamu wakati wowote Seneta mwingine anapochangia, kwa kueleza kwamba anasimama kwa Hoja ya nidhamu na atahitajika kuitaja Kanuni ambayo inakiukwa.

Nimekusomea Kipengele cha 93 katika Kanuni zetu za Kudumu na nimeona ya kwamba kumeanza kuwa na uzoefu. Nilimskia Sen. (Dr.) Zani akijaribu kuzua Hoja ya nidhamu lakini hakuskizwa. Hapo awali hata mimi nilipitia hayo. Sijui kama Kanuni hii imebadilika kwa sababu inasema kwamba Mbunge yeyote anaweza kuibua Hoja ya nidhamu wakati wowote ambapo Seneta mwingine anachangia kwa kueleza kwamba anasimama kwa Hoja ya nidhamu na atahitajika kuitaja Kanuni inayokiukwa. Hakuna mahali inasema kwamba Spika ataamua kama atampa nafasi ama hatampa kwa sababu ni haki ya huyo Seneta kuibua Hoja ambayo yuko nayo.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Nafikiri hakuna tashwishi Sen. Sakaja kwa sababu kila mtu ambaye ameomba kutoa Hoja ya nidhamu ameweza kupatiwa nafasi ya kufanya hiyo Hoja ya nidhamu.

Lakini tusiwe na ule uzoefu wa kwamba ni lazima. Seneta wa Mombasa alikuwa amesimama kwa Hoja ya nidhamu. Kwa hivyo, hauwezi ukachukua ile nafasi kumpa Seneta mwingine pia Hoja ya nidhamu kabla ile nyingine kumalizika. Kuna utaratibu wa Bunge la Seneti na hilo ndilo jukumu la Spika. Lazima Spika aonyeshe taratibu katika Bunge la Seneti.

Lakini najua kuna ule uzoefu wa kwamba kuna Maseneta wengine ambao wanataka wakishaitisha Hoja ya nidhamu, wengine wanyamaze lazima kwanza yeye azungumze. Nafikiri hiyo sio haki. Kuna utaratibu ambao unafaa kufuatwa na mimi kama Spika msaidizi nina jukumu la kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika Bunge la Seneti.

Sen. Kang'ata, endelea.

Samahani kwa hilo. Nimeelekezwa ipasavyo. Nataka sasa kuweka swala rasmi kwamba:-

Kutokana na Kanuni za Kudumu, Kanuni ya 31(3)(a) kwamba Bunge la Seneti liweze kuazimia kuongeza muda wa Kikao hiki mpaka mwisho wa Hoja zote, Hoja ya 19 ikiwa ya mwisho katika orodha ya Ratiba ya leo.

(Question put and agreed to)

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Hoja ifuatayo. Sen. Kang'ata, endelea tafadhali.

(Resumption of debate on Statements)

STATEMENT

BUSINESS FOR THE WEEK COMMENCING
TUESDAY, 9TH FEBRUARY, 2021

Sen. Kang'ata: Mr. Temporary Speaker, Sir, pursuant to Standing Order No.52(2), I hereby present to the Senate the following status of business before the House. As you are aware, today is the last Sitting Day, pursuant to the Senate Calendar adopted on Thursday, 27th February, 2020 and recently altered on Wednesday, 11th November, 2020, pursuant to Standing Order 29.

At the rise of the Senate today, the Senate will proceed on recess until Tuesday, 9th February, 2021. With respect to the business of the Senate, the Senate had published a total of 94 Bills. Out of these Bills, 14 were assented to and 34 were pending consideration by the National Assembly most of which were deemed to be money Bills.

Mr. Temporary Speaker, Sir, however, following the judgment of the High Court in constitutional petition No. 284 of 2019, the court ruled in favor of the Senate and stated that all Bills should comply with Article 110(3) of the Constitution. This resulted in secession of consideration of all Bills that were before Parliament, which had not conformed to Article 110(3) of the Constitution.

The Senate has since complied with the judgment given by the High Court and republished nine Bills, six of which are currently undergoing concurrence.

Mr. Temporary Speaker, Sir, the offices of the Speaker and the Senate leadership have been engaging with our counterparts in the National Assembly to fast-track the process of regularizing all Bills to conform to the joint resolution process under Article 110(3).

We are optimistic that by the commencement of the Fifth Session in 2021, we will have made significant progress and the Senate will begin that session with its plate already full.

Mr. Temporary Speaker, Sir, we all appreciate and recognize the importance of Petitions as a legislative tool to undertake our mandate of oversight and representation.

I would like to bring to the attention of the Senate that a total of 109 Petitions have been submitted since the First Session, out of which 47 reports have been tabled by the respective committees to which the Petitions were committed.

Let me take this opportunity to thank the Standing Committees for this tremendous work and urge the other committees also to move with speed and conclude all Petitions and table reports as required by Standing Order No. 232(2).

Mr. Temporary Speaker, Sir, with respect to Statements, 136 have been requested during this session. Hon. Senators will recall that the Standing Orders were amended in 2019 to streamline the processing of Statements.

In this respect, Statements sought under Standing Order No. 48(1) are referred to the respective committees who are required pursuant to Standing Order No. 51 to make Statements for matters for which they were responsible and table quarterly reports on matters relating to activities of the committee.

I take this opportunity to applaud committees for their reports, which have been filed and also tabled before the Senate. I urge them to deal with pending Statements accordingly.

Mr. Temporary Speaker, Sir, with regard to Motions, a total of 81 Motions were filed in the Fourth Session. Out of this, the Senate has debated and concluded 70 of them and 11 are pending debate and conclusion including the ones listed in today's Order Paper.

It is important for Senators to note that only Motions will lapse at the end of this session. Therefore, respective movers will be required to file Notices of Motion afresh at the beginning of the Fifth Session in February 2021.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I take this opportunity to thank all Senators for the dedication and commitment they have shown in their work, in the service of the people of this great Republic of Kenya.

As we proceed for recess, it is my hope that we will all be able to meet with our constituents, spend time with our families and friends, and also rest in preparation of the coming year, 2021.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I hasten to state that as the COVID-19 global pandemic continues to persist, let us all continue to observe the World Health Organization (WHO), Ministry of Health and parliamentary guidelines and protocols for keeping safe and minimizing the spread of the pandemic.

In conclusion, being that time of the year that is associated with three important holidays in the Kenyan calendar, allow me to end by wishing all hon. Senators a happy Jamhuri Day, Merry Christmas and a prosperous 2021.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I hereby lay the Statement on the Table of the Senate.

Thank you.

(Sen. Kang'ata laid the document on the Table)

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante sana Kiranja wa Walio Wengi.

Hoja ifuatayo.

MOTIONS

THANKS FOR THE PRESIDENTIAL ADDRESS

THAT, pursuant to Standing Order No.24 (6), the thanks of the Senate be recorded for the exposition of public policy contained in the Address of His Excellency the President, delivered on Thursday, 12th November, 2020 and further that the Senate notes the following Reports submitted by His Excellency the President in fulfilment of Articles 132 (1) (c) and 240 (7) of the Constitution, laid on the Table of the Senate on Tuesday, 17th November, 2020 –

(i) The Seventh (7th) State of the Nation Address by His Excellency the President delivered at a Special Sitting of Parliament on Thursday, 12th November, 2020.

(ii) The 7th Annual Report on the Measures Taken and Progress Achieved in the Realization of National Values and Principles of Governance.

(iii) The 7th Annual Report on the Progress made in Fulfilling the International Obligations of the Republic of Kenya.

(iv) The Summary of the 7th Annual Report on the Progress made in Fulfilling the International Obligations of the Republic of Kenya.

(v) The Annual Report to Parliament on the State of National Security.

(vi) The Report on the Ease of Doing Business: Reform Milestones 2014-2020.

(vii) The Office of the Director of Public Prosecutions Consolidated Annual Report for the Financial Years 2017/2018, 2018/2019 & 2019/2020.

(Sen. Poghio on 17.11.2020)

(Resumption of debate interrupted on 24.11.2020)

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Sen. Omogeni, nafikiria ulikuwa na muda ambao ulisalia.

Sen. Omogeni: Asante sana Bw. Spika wa Muda. Nitajitahidi sana kuendelea na kumaliza katika lugha ile ya kitaifa ya Kiswahili. Nataka kumshukuru Rais kwa ile Hotuba ambayo alitoa. Hii ni kwa sababu alitueleza kwamba katika huu mwaka ambao alikuwa anatupa ripoti hii ambayo ilisomwa tarehe 12 Mwezi wa 11 mwaka wa 2020, Serikali ilikuwa imeweka mikakati ya kununua madawati ya shule 250,000.

Hii ni ili kuhakikisha kwamba watoto wetu watakapokuwa wanarudi shule mwaka ujao, watakuwa na nafasi ya kuwa na ule umbali wa mita moja na nusu. Hiyo ni ili kusiwe na madhara katika shule kupitia ugonjwa huu wa Coronavirus (COVID-19).

Bw. Spika wa Muda, nimejaribu kutembea katika Kaunti yangu ya Nyamira na nimeona kwamba kweli kuna shule nyingi sana katika Kaunti yangu ambazo bado hazijakuwa na nafasi ya kupewa madawati. Kwa hivyo, naomba wale ambao wanasimamia Wizara ya Elimu wafanye jitihada kuhakikisha kwamba madawati haya yapelekwe kwatika kaunti zote 47 zenye ziko katika nchi ya Kenya. Hatutaki kusikia kwamba madawati haya yamegawa katika kaunti fulani na kwamba kuna kaunti zingine ambazo hazijakuwa na nafasi ya kupata madawati haya.

Bw. Spika wa Muda, hoja nyingine ambayo ningetaka kuguzia katika ile Hotuba ya Rais ni kuhusiana na jitihada ambayo Serikali yake imeweza kufanya kupigana na hili janga la COVID-19. Nakubali kwamba Rais alipoanza kushughulikia ugonjwa wa COVID-19 alianza kusaidia wakenya ambao walikuwa wanaathiriwa na hili janga.

Aliweka mikakati rasmi ya kuwalinda Wakenya, haswa mambo ya kupunguza kodi na kuhakikisha kwamba watu walikuwa wanawekewa amri ya kutokutana ama kutembea kutoka kaunti moja hadi nyingine.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Ni Hoja ipi ya nidhamu Sen. Pareno?

Sen. Pareno: Bw. Spika wa Muda, sijui kama nilisikia vizuri, lakini ni kama mwenzangu, Sen. Omogeni, badala ya kusema kwamba watoto wameathirika akasema “*ku-affectiwa*”.

Katika lugha ya Kiswahili, sijawai kusikia kama kuna ngeli kama hiyo. Kwa hivyo, afadhali aitoe hiyo kutoka kwa taarifa ya Bunge, la sivyo itabidi aajibike kwa sababu ya masharti yaliyowekwa katika Bunge.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante sana, Sen. Pareno. Wewe tayari ulikuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hivyo, nafikiria umebobea katika lugha. Lakini ningependa kuwaruhusu Maseneta wenzangu kwamba tujaribu tu kuzungunza lugha. Hata kama kutakuwa na dosari, lakini kujaribu ndio kuweza.

Endelea.

Sen. Omogeni: Asante sana Bw. Spika wa Muda. Mimi nawazungumzia watoto kule Kaunti ya Nyamira na Nairobi ambao wamezoea ile Kiswahili ya *Sheng*. Nataka kuwatia moyo kwamba Serikali imeweka mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba wakirudi shuleni mwaka ujao, hawatakuwa kwenye hatari ya kupata ule ugonjwa wa COVID-19.

Nikimalizia kuhusu COVID-19, ningemuomba Rais wetu aangalie upya ile mikakati ambayo imewekwa kuthibiti huu ugonjwa wa COVID-19, haswa wakati huu ambapo tunaelekea katika ule msimu wa Krismasi. Kutakuwa na watu wengi ambao watakuwa wanakusanyika wakiwa katika sherehe za kuburudika na familia na marafiki.

Bw. Spika wa Muda, lakini hatari yenye iko ni kwamba, wataki ambao watu wanakusanyika wakiwa wanafanya sherehe na kuwa katika sherehe za maankuli, huo ndio wakati ambao kuna hatari kubwa sana ya kusambaza huu ugonjwa wa COVID-19.

Nataka niombe kwamba pia Rais atakaporejea tena Bungeni mwaka ujao, atueleze shughuli ambayo Serikali imefanya kupigana na janga la COVID-19. Ni vizuri kwamba, Serikali iangalie upya ile mikakati ambayo inaweza kuwekwa wakati huu wa msimu wa Krismasi. Hii ni ili tuweze kudhibiti zaidi huu ugonjwa wa COVID-19.

Bw. Spika wa Muda, kumbuka kwamba mwaka ujao kutakuwa na wanafunzi wengi ambao watakuwa wanarejea shuleni wiki ya kwanza ya mwezi wa Januari mwaka wa 2021. Ni vyema tuweze kuzuia kueneza huu ugonjwa ili kuhakikisha kwamba, watoto ambao watakuwa wanaenda shule mwezi wa kwanza mwaka ujao, wasiende kama wamepata ugonjwa wa COVID-19.

Bw. Spika wa Muda, hii ni kwa sababu itakuwa ni hatari sana kwa wanafunzi wengine kupata ugonjwa huu haswa walimu. Pia ni vizuri Serikali zetu za kaunti zihakikishe kwamba zimeweka mikakati ya kuwa na vitanda vya kutosha vya kulaza wagonjwa mahututi. Hii ni kwa sababu tukishamaliza huu msimu wa Krismasi, kuna hatari kwamba ugonjwa huu utapata tena mchangamko wa kuenea zaidi katika taifa lote.

Pia namshukuru Rais kwa hiyo Hotuba ambayo alizungumza kuhusu maneno ya Building Bridges Initiative (BBI). Nia yake ni kuwaunganisha Wakenya na kuhakikisha kwamba sisi sote tunaenda mbele kama taifa.

Bw. Spika wa Muda, ningependa kumshukuru sana kiongozi wa taifa pamoja na kiongozi wa chama cha Orange Democratic Movement (ODM) aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga. Hii ni kwa sababu walihakikisha kwamba baada ya kupokea maoni kutoka kwa wananchi, ile ripoti ambayo tumeipata sasa ya BBI imeshughulikia mikakati ama mchangamko ambao Wakenya walikuwa wamezua kuhusiana na ile ripoti ya kwanza.

Nikizungumza kama Seneta wa Kaunti ya Nyamira, nataka niwashukuru sana. Hii ni kwa sababu tulipopata hii ripoti mara ya kwanza sisi hatukuwa tumeongezewa eneo Bunge katika kaunti yetu ya Nyamira. Lakini baada ya wengine wetu kuteta sana na kusema kwamba hatungekubali hii BBI kama hatungekuwa na eneo Bunge limeongezwa kule Kaunti ya Nyamira, nafurahi sana kusema kwamba sasa Kaunti yetu ya Nyamira imeongezewa eneo moja la Bunge. Ikiwa BBI itapita, sisi watu wa Kaunti wa Nyamira tutarudi hapa tukiwa na eneo Bunge na wawakilishi watano na sio wane.

Pia nafurahi sana kwamba Kipengele 11 sasa kinaongea kuhusu maneno ya kilimo. Ni kwamba wakulima wetu wa chai sasa watahughulikiwa na Serikali. Kule Nyamira, ukishughulikia mkulima wa chai na uhakikishe kwamba anapata mapato yake vyema haswa malipo ya chai ikiwa imewekwa kwa Kshs50. Sisi ndio tutakuwa mbele katika huu wimbo wa *reggae* kuliko watu wengine nchini Kenya.

Tunashukuru Serikali yetu kwa kuhakikisha kwamba kutakuwa na mikakati ya kushughulikia mahitaji ya wakulima wa chai, ili wasiendeleo kugandamizwa. Inafaa tufuate yale ambayo Rais alituambia katika Hotuba yake; kwamba, tumalize hali ya umasikini ili Wakenya wapate mapato ambayo yanawafanya waonekane kama binadamu. Ni lazima tushughulikie mkulima.

Bw. Spika wa Muda, hata ukiangalia maneno ya kilimo ya mimea kama kitunguu, wakulima hawapati soko la bidhaa yao. Hii kwa sababu wale wakulima kutoka Tanzania ndio wanaleta vitunguu kuuza katika soko letu hapa Kenya.

Ukiangalia upande wa mayai, mayai mengi ambayo tuko nayo hapa Kenya yanatoka kule nchi jirani ya Uganda. Ni sharti tuweke mikakati ya kuhakikisha kwamba tunamtetea mkulima.

Bw. Spika wa Muda, kule Marekani wakati hili janga la COVID-19 lilitokea, yule Rais ambaye anaondoka; Bw. Trump, aliweka kando karibu USD19 bilioni ili kuhakikisha kwamba hasara kwa mkulima inapunguzwa.

Hapa Kenya pia ningependa kwamba Serikali iweze kuweka mikakati ya kusaidia mkulima ili kupunguza hasara ambayo inawezakutokea na hili janga la Coronavirus disease (COVID-19).

Bw. Spika wa Muda, katika usambazaji wa umeme, namshukuru Rais vile alituambia kuwa Wakenya wengi sana sasa wamepata nafasi ya kupata umeme. Tangu Serikali ambayo tuko nayo sasa ichukue hatamu ya uongozi, kuna maeneo kadhaa ambayo yamefaidika sana na kuunganisha umeme kwa wananchi wa nchi yetu ya Kenya.

Shida ambayo iko ni kwamba ile kampuni ambayo inashughulika maneno ya kuunganisha umeme kwa wananchi, yaani, Kenya Power Company haina uwezo wa kuwafikia Wakenya wote.

Hata sehemu ambazo imewai kuunganisha Wakenya saa zingine kukiwa na kasoro katika ile mitambo ambayo inasambaza umeme ambayo tunaita *transformer*, inachukua muda mrefu sana kurekebisha mitambo hiyo ama kuleta ingine mpya wakati inaharibika.

Bwana Spika wa Muda, kwa mfano, kule eneo Bunge langu la Mugirango Kaskazini katika Kauti ya Nyamira kuna *transformer* ambayo iliharibika karibu miezi miwili iliyopita. Ni kule katika shule moja inaitwa Gekendo, karibu na Soko la Obwari. Hii ni kwa sababu hii kampuni ya Kenya Power Company hata kama tumeipatia jukumu la kuunganisha umeme kwa Wakenya, imeonyesha wazi kwamba haina uwezo.

Wakati umewadia ambapo inatakikana tukubali kwamba kampuni ingine ije ili iweze kusaidia katika hii shughuli ya kuunganisha umeme katika maeneo mbali mbali katika taifa letu la Kenya.

Bwana Spika wa Muda, katika maneno ya kupigana na umasikini na upweke kwa vijana, namshukuru Rais vile amesema sasa hivi hapa Kenya tuko na wale vijana ambao wanafanya kazi ya *boda boda*. Wanazidi sasa million moja nukta nne. Hao vijana wenyewe wanaleta katika uchumi wa taifa letu karibu Kshs357 bilioni.

Lakini pia kuna shida ambayo inawakumba hawa vijana. Hawa vijana katika zile sehemu za mashambani--- Seneta wa Kaunti ya Nairobi anaweza kutueleza, lakini kule mashambani wanasumbuliwa sana na maaskari. Mara nyingi hao vijana wakiwa wanafanya biashara zao wale askari ambao wameweka vizuizi barabarani wanawaitisha Kshs50 kila wakati wanapopita katika vile vizuizi.

Bw. Spika wa Muda, vile Rais amesema, angetaka kuona kwamba hao vijana uchumi wao iweze kuinuka siku zijazo wawe hata na makampuni ya kutengeneza *boda boda*. Lakini itakuwaje kwamba ile juhudi ambayo Serikali yetu inaunga mkono sana inawekewa pingamizi na maaskari wetu?

Nataka kuomba Serikali yetu ihakikishe kwamba wale maaskari ambao wako katika mabarabara zetu kazi yao isiwe kusumbua wale vijana ambao wanafanya kazi ya *boda boda*.

Bw. Spika wa Muda, nataka nikuambie kwamba hata Ijumaa iliopita nilikuwa katika Kaunti yangu ya Nyamira nikitembea kutoka soko moja inaitwa Ikonge, nikatoka katika barabara nyingine inatokea katika kampuni ya Kipkebe. Hapo kati kati, kuna maaskari wameweka kizuizi. Hao vijana wanasema kuwa kila mara wanapopita pale wanatoa kodi ya Kshs50. Wengine wanatoa Kshs100.

Huo sio ungwana kabisa. Baadhi ya vijana hao wamesoma sana lakini wanafanya kazi ya *boda boda* kwa sababu Serikali yetu haijaweka mikakati ya kutosha ya kupata ajira ya kutosha kwa vijana wetu.

Bw. Spika wa Muda, naomba Mkuu wa idara ya polisi ahakikishe kwamba mambo ya kutesa hawa vijana ambao wanafanya kazi ya *boda boda* ikome kabisa. Sio ungwana tena kuona vijana kama hao ambao wanajaribu kutafuta riziki kwa familia zao--

-

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Je, unataka kuarifiwa Seneta?

Sen. Omogeni: Bw. Spika wa Muda, ningependa. Nampa nafasi rafiki yangu, Seneta wa Kaunti ya Nairobi.

Sen. Sakaja: Asante Bw. Spika wa Muda. Ningependa kumuarifu Seneta wa Kaunti ya Nyamira. Namshukuru kwa nafasi hii. Ni kusema kwamba ni Hoja ya arifa. Ni kweli kuwa pia vijana wa Nairobi mara nyingi wanasumbuliwa na kunyanyaswa na maafisa wa polisi, lakini wanajitafutia riziki. Hivi leo kuna vijana wangu wengi ambao wanafanya kazi ya *boda boda* na pia wale wa matatu.

Ukiagalia upande wa Ruai, Njiru na Kayole kuna Forward Travellers Sacco wa matatu na wale wa Outer Ring na Eastern Bypass wameshikwa wengi. Wamewekwa kwa

“mariamu” jinsi tunaita ile lori. Wamejazwa na kushikwa bila kuzingatia kanuni za kupigana na COVID-19. Pia Nairobi tuna shida kama hiyo.

Nafikiria hiyo shida ya Nyamira iko zaidi. Nimefurahi kwamba mimi na wewe na Kamati yetu tutaenda Nyamira wiki ijayo kuangalia. Itabidi pia tuangalie mambo kama hayo. Wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Haki. Tuko tayari pamoja na Maseneta wenzangu, Sen. Olekina, Sen. Mutula Kilonzo Jnr. na wale ambao wako katika Kamati hiyo. Sen. Olekina atakuja kama jirani wa Nyamira. Tutakuja kuzungumzia vijana na kuwapa moyo ya kwamba kupitia Building Bridges Initiative (BBI) kuna nafasi yao itapatikana hapo.

Sen. Omogeni: Bw. Spika wa Muda, nimefurahi sana na hiyo taarifa ya kujulishwa na Seneta wa Nairobi. Kwa hakika ni aibu sana kuona kwamba maaskari wetu ambao wanatakikana kutulinda na kuhakikisha kwamba wale wanafanya biashara hawatishwi, ndio wanawatesa vijana wetu.

Nafikiri kama Mwenyekiti wa Kamati wa Haki wiki ijayo sisi tutafunga safari hadi ofisi ya Ethics and Anti-Corruption Commission (EACC). Hii ni ili tujue ni jitihada gani zitawekwa na ile ofisi kuhakikisha kwamba maaskari wetu ambao wako katika barabara zetu na vizuizi hawawatesi vijana wetu wa *boda boda*.

Bw. Spika wa Muda, hii ni kwa sababu hakuna haja ya kukubalia kitengo cha polisi kuwatesa vijana wanaotea nchi yetu Kshs357 bilioni. Ni lazima tumuite Mkuu wa polisi na kitengo cha kupigana na ufisadi watueleze ni mikakati gani wameweka kuhakikisha kwamba hawa vijana ambao wanafanya kazi ya *boda boda* hawaendelei kufanyiwa dhulma na polisi katika vizuizi.

Nikiendelea pia nataka kumshukuru Rais. Amesema kwamba hii shughuli ya BBI vile tunaendelea mbele tukubali kwamba tuzungumze kama Wakenya. Mheshimiwa Rais ametuambia kwamba ile sheria ambayo imechapishwa na kuwasilishwa katika Bunge la Taifa ya kushughulikia maneno ya kura ya maoni--- Amesema kwamba tuangalie sheria hiyo ili tuweke mikakati ya kusaidia taifa hili kuenda mbele na kufanya kura ya maoni.

Bw. Spika wa Muda, tangu tupitishie Katiba yetu ya 2010, nchi hii haijawai kufanya kura ya maoni. Hii ndio mara ya kwanza kabisa tunaenda katika kura ya maoni. Mheshimiwa Rais ametusihia kwamba hii sheria ya kura ya maoni ikija kwetu, tuingalie na tuifanyie ukarabati kabisa. Tuwape Wakenya nafasi watueleze ni vipi tunaweza enda kwenye kura ya maoni tukitumia sheria hii.

Ningeomba Maseneta wenzangu kwamba tuangalie vile nchi zingine zinafanya. Mwaka 2008 nilipokuwa mwenyekiti wa Chama cha Wanasheria nchini, nilisafiri mpaka kule Marekani wakati kulikuwa kunafanywa uchaguzi kule. Niliona kwamba katika uchaguzi wao, vile wanafanya uchaguzi wa kuwachagua viongozi, pia unapata kwamba kuna maswali pale yamewekwa ya kura ya maoni.

Bwana Spika wa Muda, ukitembea katika kule nchi ya Australia, wananchi wanapewa nafasi ya kufanya mjadala. Swali ya kura ya maoni ikiwekwa kwenye wananchi wanapewa nafasi ya kuchagua.

Nataka niwaombe machifu wetu na manaibu wa chifu kwamba hii maneno ya kura ya maoni inaungwa mkono na Wakenya wengi. Hakuna haja hawa manaibu wa chifu wajaribu kuwadhulumu Wakenya wenzao. Hii sheria tutaenda kule na kuongea na watu wetu kule tunatoka na tutaipitisha kwa amani.

Hatutaki Wakenya washurutishwe. Huu ni mjadala ambao uko na wafuasi wengi. Tungetaka Wakenya wapewe nafasi yao waweze kuchukua hatua ya kidemokrasia. Kuna

wengi ambao wataipigia kura. Kuna wale wanaoipinga, ambao nafikiri ni wachache. Wakiikataa basi hiyo pia ni demokrasia.

Tumepata eneo Bunge mpya katika jimbo la Nyamira. Tumeambiwa kuwa mambo ya wakulima wa majani chai watashughulikiwa. Kwa hivyo, tutaungana na Wakenya wengine kuhakikisha kwamba tunawapatia wetu nafasi ya kusoma vitabu vya the Building Bridges Initiative (BBI). Wakiona kwamba wanafurahishwa na wanafaidi kutokana na mapendekezo yote kama kuongeza pesa kutoka asilimia 15 hadi 35 katika Majimbo, waunge mkono. Wakiona kwamba ni vizuri kwa sababu tumeweka maneno ya Ward Fund katika Katiba, watasoma na wakiona kuwa ni sawa watapiga kura. Hiyo ni demokrasia.

Kwa kumalizia, Hotuba ambayo Rais alitoa inatupa changamoto kama taifa kuunga Rais wetu mkono kuhakikisha kuwa Kenya inasonga mbele ikiweka Wakenya pamoja. Nimefurahi jinsi Rais alivyosema kuwa tumerahisisha maneno ya kusajili kampuni. Kila siku tunasajili zaidi ya kampuni 300. Shida ambayo tuko nayo ni kuwa wale wakuu wa majimbo, magavana, hawapatii vijana na kina mama wetu nafasi ya kufanya biashara. Unakuta kuwa wamama na vijana wamefanya jitihada ya kusajili kampuni zao lakini ukienda kwa serikali ya majimbo uulize vijana au wamama wangapi wamepewa nafasi ya kufanya biashara katika kaunti hakuna. Wale wachache ambao wamefanya biashara wakienda kutafuta malipo yao wanaambiwa watoe rushwa, inaitwa '10 per cent.'

No side was a loser, every side was a winner. Eventually, Kenyans have settled on a formula which will help us to move forward.

A lot has been said against the BBI. However, at the end of the day, I say this with full knowledge that I sat in Serena Hotel and saw the difficulties that we had during the post-election violence.

The promulgation of the 2010 Constitution was as a result of the events and discussions that enumerated out of the Agenda 4 which generated so much interest for Kenyans and gave us a wonderful Constitution of Kenya, 2010.

After the promulgation, it was quite clear that we still needed to amend some Articles of the Constitution to re-align it with the new interests of Kenyans particularly the marginalized groups, for example, the youth and the county governments that were not receiving enough resources.

For me, the take away in BBI is the 35 per cent of the national revenue to be shared with the county governments. It will not be on the basis of the recently adopted accounts of 14 or 15 per cent which was little money going to the county governments. It will be based on the recently adopted Auditor-General's accounts.

The second take away is the youth commission which will cascade all the way to the ward level.

The third take away is the Ward Fund which we all fought for in the Senate. We agreed and it went to the National Assembly who could not agree. Fortunately, it has

found its way to the Constitution. I am quite happy that it will be something that we will live for.

I have always yearned for a time when this country will never go to war or into a crisis because of our politics. Therefore, I am glad that we will do much in this new BBI process. Let us embrace it all together. I have already signed for it and many people are signing for it. We should create a spirit of willingness for all of us to move together to the future without any doubt.

I do not want to say much about public accounts because my colleagues want to contribute also.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante sana.

Sen. (Prof.) Ongeri: Mr. Temporary Speaker Sir, with those few remarks, I second this Motion on Adjournment.

(Question proposed)

Sen. Cherargei: Asante, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono Hoja hii ambayo imeletwea na Mratibu wa walio Wengi.

Nina mambo mawili---

Sen. Madzayo: Nina hoja ya nidhamu, Bw. Spika wa Muda.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Una Hoja ipi, Sen. Madzayo?

Sen. Madzayo: Bw. Spika wa Muda, kwa unyenyekevu, taadhima na imani kuu tulionayo juu yako, tunataka hii hoja ya nidhamu, kwa sababu tunaenda likizo, ndipo tukaongeza muda kidogo ili tueleze matumaini yetu katika Bunge letu la Seneti kama alivyosema Mratibu wa Walio Wengi Katika Seneti---

Ninigependelea badala ya dakika mbili - kwa vile tumebaki wachache - tupate kama dakika saba ama nane kila mtu.

(Applause)

Asante, Bw. Spika wa Muda. Nina imani na uhakika kwamba utakubaliana na mimi.

The Temporary Speaker (Sen.(Dr.) Mwaura): Kwenye orodha yangu hapa, nina Maseneta wanne ambao nitawapa kila mtu dakika tano. Nimekubali kwa sababu pia ya weledi wa lugha na umahiri wako na vile ambavyo una haiba nzuri.

Sen. Cherargei, kijana mtanashati, una dakika zako tano.

Sen. Cherargei: Asante Sana, Bw. Spika wa Muda, kwa nafasi hii.

Kama nilivyotanguliza hapo awali, ninaunga mkono Hoja hii ambayo imeletwa na Mratibu wa Walio Wengi Katika Seneti. Hii ni mara ya kwanza kuunga Hoja ambayo ameleta kwa sababu tunaenda likizo.

Nina mambo mawili tu. Kwanza ni kuhusiana na kazi ya Bunge la Seneti. Tumejaribu pakubwa kulingana na vile ambavyo tumepewa katika Ibara ya 96 ya Katiba yetu ya Kenya. Tumejaribu kufanya yale yaliyokuwa mbele yetu na yale ambayo yametendeka.

Huu ulikuwa wakati ambapo uhuru wa Seneti na Bunge la Taifa uliangamizwa na Serikali ya Taifa. Ninakumbuka wakati huo ndio Mratibu wa Walio wengi katika Seneti, Sen. Kang'ata, alikuwa anafanya kazi hiyo. Nimeshukuru sana kwa kusikia Ripoti ya

Kamati ya Haki, Masuala ya Sheria na Haki za Kibinadamu wakizungumziwa hapa. Wakati huo ilikuwa jambo la heshima sana kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo katika Seneti.

Tumejifunza mambo mengi. Kwanza, uhuru na demokrasia ya Seneti na Bunge la Taifa lazima umepewe nafasi kwa mujibu wa Katiba ya Kenya. Wenzangu wanapofurahia viti, kama vile ndugu yangu Kiranja wa Walio Wengi katika Seneti na Viongozi wa Walio Wengi katika Seneti, wajuwe ya kwamba raha ni kidogo tu. Ni lazima waambie wale wanaoogoza Serekali ya Taifa kuwa uhuru na demokrasia wa Seneti na Bunge la Taifa lazima uheshimiwe.

Pili, ni kuhusiana na ile kesi tuliopoleka katika Mahakama Kuu Zaidi Nchini. Nimefurahi kuwa uhuru wa mahakama zetu ulionekana. Bunge la Seneti limepewa nafasi bora ya kujiimarisha na kuheshimika hasa wakati tunapotunga Sheria katika Seneti na Bunge la Taifa.

Siwezi kujisifu lakini wakati huo nilikuwa Mwenyekiti na weledi wangu ulionekana. Ninafurahi kuwa katika historia ya Bunge la Seneti itajulikana kuwa Seneta wa Kaunti ya Nandi, Sen. Cherargei, alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Masuala ya Kisheria na Haki za Binadamu. Inaonyesha kama wangukuwa wanatumia weledi, umahiri na uongozi bora katika Kamati za Seneti, ningekuwa ninaendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

La tatu na la mwisho, nimemsikia mwenzangu akiongea katika Hoja hii kuwa BBI inashughulikia--- Ninaomba Taifa letu la Kenya tuweze kutimiza malengo na azma ya Katiba ya 2010, ili kila Mkenya apate haki. Kama tutatekeleza Katiba hiyo asilimia mia kwa mia, hatutakuwa na haja ya kuja na mchakato wa BBI ambapo watu wengine hawajakubali kuwa wameshindwa katika uchaguzi.

Ninapooona Mwaka wa 2023 na kwenda mbele, tumeanza kasumba ambayo haitakuwa nzuri katika demokrasia ya taifa letu la Kenya.

Wale watakaoshindwa katika uchaguzi wa urais ama uchaguzi mwingine, watakuwa wanatumia *handshake* ama maridhiano kama njia ya kuingia katika uongozi.

Sijafurahia mchakato wa Building Bridges Initiative (BBI). Ikifika wakati huo, nitapinga. Hii kwa sababu haijapata ile azima na dhamira ya Wakenya. Uchumi wa taifa letu la Kenya hauwezi kukidhi ama kubeba ule mzigo ambao Wakenya wataongozewa. Kwa mfano, tutakuwa na Bunge kubwa ambalo tutakuwa tunalipa Ksh20 bilioni. Uchumi wa Kenya umekuwa uchumi wa mtumba. Uchumi ambao hauwezi kupanua Serikali ya kitaifa, na Bunge la Kitaifa na Seneti.

Bw. Spika wa Muda, nashukuru sana. Naunga Hoja hii.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante sana, kijana, Sen. Cherargei, kwa wasifu uliojipa. Waswahili wanasema, ngoja usifiwe.

Sen. Olekina, naomba uzungumze.

Sen. Olekina: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir, I rise to support this Adjournment Motion.

Let me begin by saying that I am a very proud Senator of the Republic of Kenya. I am proud of my colleagues including Sen. Stewart Madzayo, my senior, Sen. Faki, my brother also senior, Sen. Sakaja Johnson, “*Super Senator*”, for having come together to show this country a direction that we cannot achieve anything when we only think about our stomachs without thinking about the rest of the 47 million Kenyans.

Mr. Temporary Speaker, Sir, “*Team Kenya*” did a fantastic job to fight for revenue to be sent to the counties and ensure that no county lost any coin from what they had been allocated in the previous year.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I also would like to thank my colleagues who came and joined us like Sen. Cherargei and my good friend, “*my ganja man*”, Sen. Irungu Kang’ata. Earlier on, when he was moving---

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Samahani, Sen. Olekina, unamaanisha nini ukisema “*my ganja man*.”

Sen. Olekina: Hilo ni jina tunaitana. Haina maana yeyote.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I was amused by my good friend, Sen. Irungu Kang’ata, because he rose to move a Motion and he did not sign that report. Some of these things are very interesting. I will let that slide.

I am quite happy with the work that this Senate did. 14 Bills were assented to by the President. That is good work for this Senate.

Mr. Temporary Speaker, Sir, on the issue of the BBI, I want to be very clear that when we worked as “*Team Kenya*” and eventually as 12 wise men and a lady who came together to give this country a direction, one of the things that we are trying to defend is Article 203 of the Constitution.

During this time, when we are going on recess, it will give us an opportunity to explain to our constituents and particularly myself, why I have serious reservation with the Constitution Amendment Bill.

Mr. Temporary Speaker, Sir, Article 203 of the Constitution relates to the issues of the Consolidated Fund. The amendments which are being proposed by the Constitution Amendment Bill will negate all the gains that we made in this House fighting for the revenue formula. That is one of biggest beefs with this Constitution Amendment Bill. There is no point of having sat here, burnt the midnight oil and then at the end of the day, we still divide the country by bringing the argument of “one man one vote one shilling.”

Mr. Temporary Speaker, Sir, my heart bleeds for the people of Lamu. When this Bill goes through, they will be denied money.

My heart bleeds for the people of Samburu whom when this Bill passes they will be denied some money. It saddens me that this Senate will no longer have voting powers to determine any matter because of the deletion of Article 123. We must explain these things to our people in our constituencies. Sir Winston Churchill once said, “Mountain tops inspire leaders, but valleys mature them.”

I believe that we have all matured in this House to a point where we want a country that will think about the 47 million Kenyans and not just a small section of the Kenyans. It is my prayer that this contentious Bill, the amendments to Article 203 will be removed. I do not know if we will have the opportunity to do so.

If we do away with the provisions or amendments of Article 203, we can support all these other things. I wish it had been put into legislative proposals because it could be changed at any time.

Yesterday we went to Naivasha because of a serious matter that relates to Narok County. In many instances, my people get frustrated when their cows are knocked down by fast moving vehicles on Mai Mahiu-Bomet Road. We agreed the road will not be closed whenever our cows are knocked down, but I urge Kenyans who use that road to be more cautious and allow cows to have the right of way.

There is also an issue of land disparity. Land has been taken away from the Maasai people. I believe that going back home, we can talk about this issue of land.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante sana. Muda wako umeisha. Nampa nafasi Sen. Sakaja.

Sen. Sakaja: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. I support the adjournment Motion. I really yearn for the day when Parliament will live up to its billing. The name Parliament comes from the Latin saying of parlance, which means to speak. When we are in Parliament and we are told to speak for two minutes or four minutes, yet we are here to speak and we have moved an adjournment Motion until we finish all the business. It goes against the reason.

Mr. Temporary Speaker, Sir, when you and I were in the National Assembly, we used to admire the Senate because of the quality of debates because Senators would speak. In the National Assembly, it was almost like a high school where you are given two minutes and you cannot even pass a point. Sen. (Prof.) Ongeru has years of experience. I want to hear Sen. (Prof.) Ongeru speak for 10 minutes. The late Martin Shikuku used to speak for three hours. I have spent a minute speaking that.

In this session, we have lost Kenyans to COVID-19. However, I would like to ask that we acknowledge frontline health workers who have been at the forefront of fighting COVID-19. They have been doing an amazing job. May souls of those who lost their lives during this fight against COVID-19 rest in peace. A few of our colleagues in the National Assembly have lost their lives and may their souls rest in peace.

As of today, Kenyans have lost thousands to this pandemic and are still dealing with this pandemic. In this session, the Senate has been able to come out strongly in terms of oversight not just on the pandemic, but also on county governments.

It has been a tough year in many respects, but it has been a year of growth. It has been a year where we have been seen to do our work as a House---

It has been a year of growth and where we have been seen to do our work as a House. Sen. Olekina acknowledged the work we have done, not just from 'team Kenya' but across the isle as Sen. Kang'ata said. We reestablished the place of this House because of two things. Number one, the amendment of the formula. It was not on population; Nairobi has the highest population but was number 28. With what we did we were able to get our rightful share based on not just population but other factors. If you add the BBI's proposed 35 per cent, counties from the next year if it is passed next year before the next financial year get Kshs475 billion. This is 35 per cent of the last audited revenue of Kshs1.3 trillion, whose 35 per cent is Kshs475 billion. Nairobi county will get Kshs25 billion. Narok County will get Kshs10.8 billion. Kilifi County should get Kshs14.4 billion. Kisii County should get Kshs11.2 billion under BBI.

Sen. Olekina: Mr. Temporary Speaker, Sir, on a point of order. I want to clarify one thing. My dear brother who I feel bad interrupting, we need to be factual. Today we have read in the dailies that the National Treasury is seeking to defer the payment of interest on T bills. Counties are claiming that they have not received money. Let us be practical. I concur with Sen. Sakaja, when he talks about parliament being given opportunity to speak and talk about this issue.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Seneta, hoja yako ya nidhamu ni ipi?

Sen. Olekina: It is on the issue of the content of the debate. The issue here is my good friend Sen. Sakaja said that when we pass this amendment-- I am on a point of order, Sen. Faki, when the BBI passes counties will get money. I want to understand why we have a challenge currently on paying interest on Treasury Bills and sending money to counties. Let us not bite what we cannot chew.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Sen. Olekina, kusema kweli hapo hakukuwa na hoja ya nidhamu. Nafikiri ulikuwa unachangia tu. Sen. Faki singalikupatia nafasi kwa sababu ilikuwa hoja ya nidhamu. Sen. Sakaja unaweza kuendelea.

Sen. Sakaja: Thank you, Mr. Speaker, Sir. The point of order by Sen. Olekina is neither here nor there. I understand what he is saying because of the pressure on the exchequer. What I am talking about is what is allocated. If this Government wants to give Kshs474 billion from Kshs3 trillion budget, they can realign the national Government budget. What the Members of Parliament do not know because they talk about the National Government-Constituencies Development Fund (CDF) being put there, it will be less. When you remove 35 per cent which is a percentage of that, add 70 counties you are dividing a smaller amount by many more. We support for the sake of our counties to get enough money.

Nairobi was getting Kshs100 million in the first bad formula that was brought. I moved that to an addition Kshs3.3 billion. With BBI plus the formula we are going to Kshs25 billion. We passed the Sectional Properties law, that if you have improved a piece of land and you have built apartments each of them is going to pay the correct rate they are supposed to pay. The revenue of Nairobi County has the potential of going to Kshs100 billion and we will sort out our problems. Part of the reason I have worked with BBI is that they have acknowledged that given a second chance and resources and right leadership Nairobi County can be governed properly.

Initially, before we amended the BBI report, it was solving a temporary problem, that of Hon. Sonko and Hon. Kidero with a permanent solution of removing devolution from Nairobians who will still have the right. We were born in Nairobi; I was born 2.3 kilometers from here. My county is Nairobi. If you tell me to look for devolution elsewhere, I do not know any other place. I speak English and Swahili and six languages because all my neighbors are from all communities. This is our home and we have the same right to devolution as the people in Kisii, Narok and Kilifi.

Sen. Olekina has spoken about Article 203 and I want to advise him. We will have a basketball tournament. We have agreed to do a one on one challenge and I will defeat him. Even as we do that, Article 203 that is being proposed in the BBI is impractical but there should be no fear.

When you talk about per capita capped by three times, if you remove the amount from those that go beyond three and redistribute it, it gives you what we call in Mathematics, a cyclic error. This is because the amount you will redistribute will be three times of that per capita. It is an aspirational clause. As you do it, try and reduce the per capita discrepancy, which is what we appeal.

Mr. Temporary Speaker, Sir, for instance, Nairobi County has been getting Kshs3000 per capita. One Nairobiian gets Kshs3000, while one person in Lamu gets Kshs20,000. We want to move towards a better per capita. The variance should not be as wide, but we cannot put it to be three times more. The long and short of it is that, despite the fact that we support a proposal that will bring us together---

As I finish, let me say that the Building Bridges Initiative (BBI) is not a perfect document. The only perfect document is the Bible. However, every generation must do what it must to actually advance or progress our unity as Kenyans. Right now, it is not perfect, but it is the best thing that we can do for the unity of this country. The next generation and the next Parliament will have an opportunity to improve on it. We cannot waste and squander this opportunity for a united Kenya. That is why we support the BBI-

--
The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante Sana, Sen. Sakaja. Sasa hivi nitampa nafasi Sen. Faki.

Sen. Faki: Asante, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa fursa kuchangia Hoja ya kuahirishwa kwa Seneti kwa sherehe za Krismasi na mwaka mpya.

Kwanza, ninapongeza Seneti kwa kazi ambayo tumefanya. Kazi hii imeangaziwa na Mratibu wa Waliowengi. Kwa hivyo, sitaguzia kila kitu tumefanya.

Vikao vya mwaka huu vimeshuhudia mabadiliko ya uongozi wa Seneti kwa upande wa Waliowengi. Tulipata kiongozi mpya wa Waliowengi pamoja na Wenyeviti wa karibu Kamati zote za Seneti. Pia mimi nilibahatika kuchaguliwa kama Mwenyekiti ywa Kamati ya *Delegated Legislation*, ambayo kwa hakika si jambo la kulichukulia mzaha. Ni jambo kubwa kwa sababu ninaweza kukaa katika Kamati ya *Liaison* na kutoa mchango wangu katika hili Bunge.

Bw. Spika wa Muda, yale madabiliko ya uongozi yameleta sura mpya katika Bunge, kwa sababu Maseneta kutoka upande wa Waliowachache wamepata fursa kuwa viongozi wa Kamati tofauti tofauti. Ninazungumzia Kamati ya *Justice, Legal Affairs and Human Rights*, Kamati ya *Devolution and Intergovernmental Relations*, Kamati ya *National Cohesion, Equal Opportunity and Regional Integration*, na pia Kamati ya *Delegated Legislation*.

Kamati hizo zote zinaongozwa na viongozi shupavu kutoka upande wa upinzani wa Seneti. Hii imeongeza *diversity* katika Bunge hili kwa sababu viongozi ambao wamechaguliwa wote ni watendakazi, na itaboresha kazi ya Bunge hili zaidi.

Ningependa pia kupongeza Bunge hili kwa kusimama kidete na kuenda mahakamani kutetea sheria zilizopotishwa bila mchango wa Seneti. Imethibitishwa na mahakama kuwa lazima sheria ifwatwe wakati Bunge la Kitaifa linapitisha sheria ambazo zitawaathiri Wakenya.

Bw. Spika wa Muda, ninafurahi kwamba tulipitisha *formula* mpya ya *third generation formula* ya ugawaji wa rasilimali za kitafia kwa serikali za ughatuzi na Serikali Kuu. Hii itachangia pakubwa maendeleo katika kaunti zetu. Kaunti ya Mombasa, ambayo ilikua inapoteza takriban Kshs700 milioni sasa imebahatika na kupata Kshs1 billioni zaidi katika mgao wa 2021/2022.

Bw. Spika wa Muda, pia ningependa kughusia hali ya nchi ilovyo kwa sasa. Sasa tunapambana na janga la Korona, tumeona kwamba huu mlipoko wa pili umekuja kwa kasi. Watu wengi wamepoteza maisha yao kuliko katika mlipuko wa kwanza.

Huu mlipuko wa pili umeonyesha dhahiri shahiri kwamba kaunti nyingi hazikuwa zimejitayarisha. Walipaka wananchi mafuta kwa mgongo wa chupa. Wengi hawakuwa wamejitayarisha. Vifaa vingi vilikua duni. Hakuna *ventilator* na vifaa vya *Intensive Care Unit (ICU)*. Kwa hivyo, watu wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya utepetevu wa serikali za kaunti na serikali kuu.

Ipo haja ya kuhakikisha kwamba kazi yetu ya kuchunguza na kuhakikisha kwamba tunafanya uangalizi ya kisawasawa kama Bunge la Seneti unaendelea katika mwaka ujao kwa sababu hiyo ndio njia pekee ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata faida kwa kuwepo kwa Bunge la Seneti.

Bado kuna visa vya maafisa wa polisi kula hongo na kusumbua wananchi hususan wale wanaosafiri. Kwa mfano, katika Barabara Kuu ya kutoka Mombasa kuenda Lamu, kuna vizuizi karibu ishirini ambazo zinachangia kuongezeka kwa gharama ya kufanya biashara katika nchi yetu. Madereva hawawezi kupita vizuizi katika barabara zetu bila ya kuwacha chochote. Utaona pia kuna ubaguzi katika kusimamisha magari katika vizuizi hivyo. Kwa mfano, magari yanayobeba miraa na bidhaa zingine za haraka zinakubaliwa kupita kwa haraka bila kuzuiliwa kama bidhaa za kisawasawa zinazoenda kuwafaidi watu wa Lamu.

Bw. Spika wa Muda, tunapoenda katika mapumziko haya na tunapokaribia sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, watu wengi watakuwa wanasafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kwa hivyo ningependa kuwahimiza kuzingatia kanuni zilizopo za kupambana na COVID-19 hivyo wanafaa kupunguza msongamano katika maeneo watakoenda kusherehekea. Nawahimiza Wakenya pia kuangalia kwamba kuna usalama wao binafsi na usalama wa wananchi wengine kokote watakapokuwa.

Maafisa wanaohusika na kulinda usalama lazima pia wawe macho kuhakikisha kwamba wananchi wanafwata sheria na vile pia wale wanaeka vizuizi vya uongo ili kuwagandamiza wananchi katika sehemu mbali mabli kule mashambani wanapelekwa mahakamani ili kuona sheria inafwatwa.

Bw. Spika wa muda, nachukuwa fursa hii kuwatakia Maseneta wote sherehe murwa za Krismasi na Mwaka Mpya. Ningependa pia kukupongeza kwa kutilia mkazo matimizi ya lugha ya Kiswahili katika Bunge hili. Nilifurahi sana wiki iliyokwisha---

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Muda wa Sen. Faki umeyoyoma lakini ningependa kumuongeza muda kidogo ili amalize sentensi yake.

Sen. Faki: Bw. Spika wa Muda, nilifurahi sana wiki iliyokwisha kumuona kiongozi wangu wa waliowachache katika Seneti, Sen. Orenge, akizungumza kwa lugha ya Kiswahili. Sen. Orenge alizungumzia jambo muhimu ambalo tunafunzwa katika dini ya Kiislamu kwamba alama za mtu mnafik ni tatu. Ya kwanza akiweka ahadi, huvunja ahadi yake. Ya pili, akiaminiwa, hufanya hiana na ya tatu, akitoa ahadi, hawezi kutimiza.

Asante Sana, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa fursa hii.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Ilidhihirika kwamba Sen. Orenge anaweza kuzungumza vyema katika Lugha ya Kiswahili. Nimeweza kuona kwamba tangu tuanze kuzungumza katika lugha ya Kiswahili katika Bunge la Seneti, watu wengi ambao walikuwa wanadhani kwamba hawawezi kuzungumza katika lugha ya Kiswahili wanazungumza katika lugha hiyo kw ufasaha. Fauka ya hayo, Bunge la Kitaifa pia limetuiga sisi kwa sababu wameweza hata kuzindua kanuni za kudumu katika lugha ya Kiswahili iliyokuwa idhana ya Bunge la Seneti lakini wakakimbia na kuzindua kanuni zao za kudumu katika ya Kiswahili kwanza. Tunaendeleza vikao vya Bunge la Seneti katika lugha ya Kiswahili hivyo Wakenya wengi wanaweza kufuata mijadala kwa urahisi.

Ninajua kwamba wanaonukuu mazungumzo haya katika HANSARD wana changamoto lakini ninaimani kwamba tutaendelea kukuza ufasaha wetu wa lugha ya Kiswahili. Ingekuwa bora pia kama ratiba ya shughuli ya Bunge ingeweza kufasiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ninapata shida sana ya kufasiri kutoka lugha ya

Kingereza mpaka lugha ya Kiswahili. Nimejizatiti sana kufanya ufasiri lakini ni vyema kuwa na tafsiri rasmi kwa sababu hii ni lugha ya taifa na wala sio lugha ya Sen. Mwaura.

Hivi sasa ningependa kumpa Sen. Madzayo nafasi ya kuzungumza.

Sen. Madzayo: Bw. Spika wa Muda. Ningependa kukupa wewe kongole kwa sababu wewe ndiye Spika ambaye anatukuza lugha ya Kiswahili au lugha ya mama. Sisi Wapwani husema kwamba kuongea lugha ya kimombo kwa ufasaha haimaanishi unajua asili zaidi.

Wewe ni mtu anayejua asili zaidi. Kwa hivyo, nakushukuru sana na pia kukupatia kongole kwa sababu hizi sheria zetu za hapa ndani ya Bunge la Seneti unazielewa na unaweza kuzitafsiri vilivyo kwa Kiswahili. Makosa yako ni kwa sababu hakuna binadamu aliye kamili.

Bw. Spika wa Muda, mimi naunga mkono kwa mara ya kwanza Mratibu wa Waliowengi ya kwamba watu waende likizo. Likizo ni kwa sababu ukifanya kazi kwa muda, binadamu yeyote lazima apate nafasi ya kupumzika, hususan wakati huu wa krismasi. Ni wakati wa kujumuika katika familia na watu wengi pia kuwa pamoja.

Lakini katika ile hali ya kuwa pamoja tuweze kuzingatia haswa zaidi mambo ya Coronavirus disease (COVID-19). Tuangalie kwa sababu hili janga la COVID-19 limetokea katika Kenya ama ulimwengu mzima baada ya karibu karne nzima ya miaka 100.

Bw. Spika wa Muda, hivi sasa Bunge la Seneti linaenda likizo na mimi naunga mkono. Tukiwa katika likizo yetu, ni kama vile hawa viongozi wetu wanaotungoza katika taifa letu la Kenya, hususan Mheshimiwa Uhuru Kenyatta Rais wa Jamhuri ya Kenya na ndugu yake, Baba Raila Amollo Odinga.

Waliweza kufanya "*Handshake*" na hatimaye kuzindua kupeana pambaja na mkono. Halafu tukasonga mbele zaidi na kusema kwamba kuna umuhimu kuleta Wakenya pamoja. Kama tutaleta Wakenya pamoja, ni jukumu letu kuwa na kitu kama daraja. Na ile daraja wakaita BBI. Sasa ni kujenga daraja ya kuona Wakenya wote wasiangaliane kwamba huyu ni Mkikuyu, Mgiriamu, Mjalu, Mkamba, Mkisii, Maasai na kadhalika.

Bw. Spika wa Muda, kwanza nampa heko sana ndugu yangu huyu Maasai, Sen. Olekina. Alitaka kufukuzwa hapa ndani. Aliye uliza swali hilo pia alikuwa ni huyu Kiranja wetu akitaka kujua kama alikuwa amevaa sawa sawa ama la.

Lakini namshukuru Spika wetu Mhe. Kenneth Lusaka. Alisimama kidete na kusema amevaa kisawa sawa. Kwa hivyo, huyu kiongozi wa Wamaasai anayevaa namna hii na anaongea sana amevaa vizuri sana. Sijui kama kuna nguo nyingine ambayo amevaa, lakini vile alivyovaa. Tunajua vile Wamaasai wanavyovaa. Huwa wanavaa mavazi haya alafu ile mambo mengine hawakuzoea tokea wazaliwe.

(Laughter)

Bw. Spika wa Muda, hakuna katiba iliyo kamili. Nataka kusema kinagaubaga kwamba hata BBI ikiwepo, sisi tutakao kuwa tunaendelea na hata tukishaenda--- Kwa vizazi vijavyo, hakuna katika ulimwengu mzima katika ambayo iko kamili. Kwa hivyo kama tunatafuta katiba ambayo iko asilimia mia moja, haitopatikana.

Lakini kwa wakati huu ambao sisi ndio viongozi, ni sharti tufanye juhudi zozote ambazo mimi naunga mkono zaidi yaliyo ndani ya BBI. Yana uwezo ya kusaidia Wakenya kwa hivi sasa kuwaleta pamoja.

Bw. Spika wa Muda, nikisema hivyo ni kwamba katika BBI tunaona hata katika maeneo Bunge mengine, hata Kauti ya Kilifi tunayo bahati ya kwamba tumezaana kisawa sawa kama zaidi ya watu wa Kaunti ya Murang'a. Tumepata viti nine vya maeneo Bunge.

Kwa hivyo, mimi Seneta wa Kilifi nikijaaliwa na Mwenyezi Mungu nitakuwa na maeneo Bunge kama 11 inshala Mwenyezi Mungu akipenda. Kwa hivyo, naunga mkono hii BBI. Sisi sote kama Wakenya ni lazima tuwe kitu kimoja na tupendane ili Kenya iwe inaweza kuendelea mbele kimaendeleo.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Endelea kwa dakika moja tafadhali.

Sen. Madzayo: Bw. Spika wa Muda, pia nataka kuunga mkono Bunge la Seneti kwa kusimama kidete na ile "*Team Kenya*" ambayo ilifanya vilivyo usiku na mchana, kuwe na mvua ama jua. Hatawezekana ikiwa kama Wakenya watagawanyana. Tulisema kuwa haitawezekana. Kila kaunti ipate pesa yake na hatimaye tuliweza kupata.

Kwa hivyo, yale mengine ambayo tunasema yataangaliwa pole pole halafu uhusiano mwema utaendelea na kila mtu atafaidika na pesa tutakazokuwa tunapigania ziwe zinaweza kwenda katika serikali zetu za mshinani.

Bw. Spika wa Muda, la mwisho ni kwamba sisi katika hizi shamra shamra, tunasema kwamba Bunge la Seneti ni lazima pia liheshimiwe. Tunaona hivi sasa bado kuna marekebisho tunahitaji.

Lakini, hata kama yako, tukipitisha, tutayarekebisha alafu tuendelee kama Wakenya wa nchi moja ambao wanapendana hili nchi yetu ipate mafanikio.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Asante Sen. Madzayo kwa weredi wako wa lugha na kujieleza. Umewahi kusema kwamba mmezaana kuliko watu wa Murang'a. Hilo ni changamoto kwa Sen. Kang'ata. Watu wa Murang'a wana idadi moja ambayo imefanya wapate eneo bunge nzima la Kahuro, Kiharu, ambako Sen. Kang'ata aliwahi kuwa Mbunge.

Sasa hivi ninampa nafasi wakili mwandamizi, George Mbogo Ochillo-Ayacko.

Sen. (Dr.) Ochillo-Ayacko: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. The name Mbogo, where I come from, is a warrior's name. So, my family are warriors' not necessary violent ones but warriors for justice.

I thank my colleagues in the Senate and your Office for the session that we have had. We have had a healthy session and robust engagement.

I hear the so called Team Kenya celebrating the formula that we have had. I would like to tell them that the formula is a product of a vibrant engagement similar to that between a man and woman that yield to a birth of a child. So, nobody should celebrate as being the single parent of the good product of the Senate. It was the engagement of Team *Katiba* and Team Kenya that brought money flowing like rain in torrents to counties. I hope that the expectant counties will get that money. It is important that they get it.

Mr. Temporary Speaker, Sir, we are celebrating the prospects of enactment of legislation including the Constitution that are associated with BBI. It is something to celebrate. BBI is premised upon sharing of resources and building a peaceful nation.

If you recollect our engagement with the President in Naivasha, he said something that I keep on remembering. He said that he had a visit to France where he had gone to witness the signing of an agreement between a private company that was planning to put up a road in Kenya. However, they wanted one guarantee of whether we will have Kenya beyond 2020. They wanted a guarantee of peace, existence and unity.

The discussions that we are having in BBI and the fact that the hardliners are coming together and putting priority of the nation over personal interest or ambition is a step towards unifying this nation. Therefore, we must thank BBI, the President of Kenya and the people's president for coming together for the sake of the nation.

Mr. Temporary Speaker, Sir, having said that, BBI intends to share resources fairly. However, we are yet to address the enlarging of the cake. What will we share? The economy is going down because of Covid-19 and young persons are unemployed because of dwindling prospects.

So, the time has come to look at Covid-19, the economy and BBI because none will be successful without the other. We must deal with Covid-19 so that it does not eliminate us from existence. We must look at the economy so that we have something to share. If we do not have something to share, we will be violent and vicious in our competition which is unhealthy for a nation that is craving for unity.

Although the Building Bridges Initiative (BBI) is putting the framework for sharing resources, it is now time for us to concentrate on working on those resources and how to enlarge the cake and to ensure we have resources we can share.

I come from Migori County where we have fish in, agriculture and potential for its realization in abundance. My county is similar to others that are sugarcane-growing. The sugarcane farmers have been told about an "animal" called privatization. That "animal" has mutated into something called leasing. This leasing or privatization as far as the farmers are concerned want a factory that will pay them in time at the right prices for what they deliver.

The employees of Sony Sugar Company and other mills want to be paid in time. They have not been paid for the last two years. They are surviving by the grace of God. The suppliers also want to be paid on time.

I support.

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Kulingana na Kanuni Za Kudumu zetu, hilo si suala ambalo tunaweza kupigia kura. Kwa hivyo, ninawashukuru sana. Kabla ya kuahirisha kikao, nina Waraka Rasmi ambao ningependa kusoma kutoka kwa Bw. Spika wetu.

TAARIFA KUTOKA KWA SPIKA

LIKIZO YA SENETI

Waheshimiwa Maseneta watadhimiwa, kama mnavyojuwa tunapomaliza Kikao, hiki Jumanne, tarehe 1 Desemba, 2020, Seneti litakwenda kwenye likizo mpaka Jummane tarehe 9 Februari, 2021 kulingana na kalenda ya Seneti.

Ni mwaka uliokuwaje jameni? Ni mwaka ambao umekuwa wa kumbukumbu katika historia za Bunge. Ni wakati tumejizatiti zaidi fauka ya tamaduni na Kanuni zetu ili kuhakikisha kwamba tunafanaya kazi katika mazingira ambayo si ya kawaida.

Tumekuwa na changamoto nyingi kutokana na misukasuko lakini tumebaki kuwa kundi moja na familia moja ya Waheshimiwa watadhiimiwa.

Mwaka wa 2020 ulianza kwa matumaini makuu. Tulikuwa na Kikao cha faragha cha viongozi katika Mwezi Machi kupanga mipangilio ya vile ambavyo tutakuwa na ajenda ya Bunge hili, utunzi wa sheria na kadhalika. Hususan tulitaka kuhakikishi tumepea nguvu ugatuzi na kuhakikisha kwamba Kanuni zetu za kikatiba na hususan miundo-msingi inayofaa.

Vilevile, mikakati yote ambayo inafaa kuwepo imezingatiwa kwa kuhakikisha tunaweza kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba hasa jukumu la Bunge la Seneti kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba tunakidhi mahitaji ya Wakenya na wadau wetu wote.

Waheshimiwa Maseneta, tunajua kwamba kutokana na janga kuu la COVID-19 katika Mwezi huo tu wa Machi, shughuli zetu zilikuwa haziwezi kuendeshwa vizuri kwa sababu mabunge yote ulimwenguni yalianza mikakati ya kuhakikisha kwamba yanachunga kuenezwa kwa ugonjwa wa COVID-19 kati ya Wabunge wenyewe na wafanyikazi wa Mabunge hayo.

Jambo hilo lilitufanya tukaanza kuwa na mikakati maalum ya kuhakikisha tunakuwa na vikao vya kamati kupitia majukwaa ya mtandao na kuhakikisha kwamba Ukumbi wa Seneti unaweza kuhodhi Maseneta 28 pekee. Pia, ilitubidi tuweze kuhakikisha kwamba miundo msingi ya kiteknolojia imeimairishwa ili kupunguza magonjwa haya na watu wanaweza kuweka nafasi kati yao.

Hilo ni jambo ambalo hatujazoea. Itakumbukwa kwamba wakati mwengine Maseneta walikuwa wanaketi kwenye viti ambavyo havifai kukaliwa. Ilikuwa ni changamoto kuhakikisha kwamba kila Seneta ana nafasi ya kuzungumza.

Ilitubidi kuhairisha Warsha ya Ugatuzi ama *Devolution Conference* na Warsha ya Utunzi wa Sheria, *Legislative Summit* na pia vikao maalum nje ya Jiji la Nairobi kuhakikisha kwamba hatuenezi ugonjwa huu wa korona.

Waheshimiwa Maseneta, mtakumbuka kwamba Kamati ya Muda ya COVID-19 iliundwa na ilikuwa ya kipekee katika Bunge zetu mbili. Kamati hiyo ilifanya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba imetoa mikakati na kupiga msasa miradi yote kuhusu janga hili ambalo liliendeshwa na Serikali ya kitaifa na zile kaunti.

Kwa hivyo, ilitubidi kubadilisha Kanuni za Kudumu za Seneti ili tuwe na kikao cha jumla cha Kamati zetu kwa njia ya mtandao. Tunashukuru kwa sababu Kamati zetu sasa hivi zinaweza kuwa na vikao vyake kupitia mtandao, lakini ukiangalia Sehemu ya 29(a) ya Kanuni za Kudumu za Seneti hatukuweza kuwafikia lengo la kuwa na kikao cha pamoja cha Bunge la Seneti kupitia mtandao. Nataka kuwahakikishia kwamba jambo hili linashughulikiwa na Ofisi yangu.

Waheshimiwa Maseneta, jambo ambalo lilikuwa la muhimu sana katika awamu hii ya nne ni kwamba tuliweza kupitisha Mgao Wa Tatu wa Fedha katika serikali gatuzi na Ratiba ya Ugavi wa fedha kupitia Mswada huu kwa serikali zote 47 za gatuzi. Sote tunakumbuka kuafikiana kwa mgao huo halikuwa jambo rahisi. Tulikuwa na tumbojoto kila wakati tulijaribu kugawa pesa kwa kaunti zetu. Maseneta walizomeana. Wakati mwengine tulikuwa na dosari kama jambo hili lingewezekana. Tulikuwa na vikao zaidi ya kumi. Lakini kwa uvulivu wetu, kuwa na subira na kuelewena, Waheshimiwa Maseneta walifikia azimio la pamoja na kupitisha fomula ya huo Mgao wa Tatu na Ratiba Rasmi ya Ugavi wa Fedha kwenye serikali gatuzi.

Nachukuwa fursa hii kuwashukuru nyinyi nyote kwa sababu ya vile ambavyo mlivyofanya kwa ujumla na pia kila mmoja wenu kwa kuonyesha umahiri mkuu na uzalendo.

Waheshimiwa Maseneta, mtakumbuka kwamba tarehe 20 Oktoba, 2020, Mahakama Kuu ilitoa uamuzi kutokana na Athihali Nambari Mia Mbili Themanini na Nne wa mwaka wa 2019 ambao ulikuwa unatoa maswali kuu kuhusu hali ya Katiba ya Miswada yote ambayo ilikuwa imepitishwa na Bunge la Taifa bila ya kuhusisha Bunge la Seneti kuambatana na Kifungu 110(3) cha Katiba yetu tukufu ya Jamhuri ya Kenya.

Uamuzi huo wa kihistoria wa Mahakama Kuu umeweza kuzindua na kuumbua upaya namna ya utunzi wa sheria na kanuni za Bunge kwa ujumla. Uamuzi huo umeweza kuonyesha kwamba lazima Katiba na sheria zote za Kenya zifuatwe na umeipa Bunge la Seneti hadhi ya juu hususani tukizingatia mambo yote ya ugatuzi kwa ujumla.

Ni muhimu tunaposonga mbele kuhakikisha kwamba tunafuata kanuni zote na sheria zote hususan ibara hii ya 110(3) ambayo inasema kwamba lazima Maspika wote wawili waweze kuwa na hati ya kuidhinisha kila mswada kabla ya kuwasilishwa katika Bunge yoyote hususan. Hilo ni jambo ambalo linasaidia sana Bunge la Seneti kuwa na nguvu zaidi.

Waheshimiwa Maseneta, nafikiri tumepiga hatua kubwa sana kuhakikisha kuwa Bunge la Seneti limeweza kuheshimiwa na naomba muwe na subira na kuelewa wakati Ofisi yangu inapofanya kazi pamoja na Bunge la Seneti na Spika wa Seneti kuhakikisha kwamba miswada hii imeweza kuchapishwa upya kulingana na ibara ya 110(3) ya Katiba yetu.

Waheshimiwa Maseneta, ningependa kusema kwamba tumefanya kazi vyema kabisa katika awamu hii ya nne. Lakini nataka kusema kwamba tunapoingia katika awamu ya tano, tunahitaji sana kufikiria vile ambavyo tutakavyofanya kazi wakati hili janga la COVID-19 litakuwa limemalizika. Ni muhimu sana tufikirie vile ambavyo tunaweza kukuza uchumi wetu katika anga ya kitaifa na pia katika kaunti zetu zote na vile ambavyo tutaweza kufanya biashara yetu na kuendesha vikao vyetu vya Bunge hii na Kenya kwa jumla.

Kwa sababu hii, Ofisi yangu inatumai kuwa na kikao maalum tukiwa pamoja na uongozi wa Seneti ili Maseneta waweze kufikiria vile ambavyo tutaweza kuendelea na vikao vyetu na kuendesha nchi yetu hii ya Kenya. Nataka kusema ya kwamba tutakuwa tukiwasiliana kuhusu kikao hiki kabla ya kuanza awamu ya tano.

Waheshimiwa Maseneta, nachukua fursa hii kuwapatia kongole zangu kwa sababu ya kujitolea kwenye na vile ambavyo mumeweza kuhakikisha kwamba hamjatelekeza majukumu yenu hata kama kumekuwa na hili janga la COVID-19, na vile ambavyo mumehakikisha ya kwamba mumeweza kutimiza majukumu yenu ya kikatiba.

Tunapo amka sasa kuahirisha kikao hiki, nawatakia muwe na wakati mwema na familia zenu, muwe na likizo njema na pia muwe na mwaka mpya wenye mafanikio wa 2021.

Nawashukuru.

ADJOURNMENT

The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Mwaura): Waheshimiwa Maseneta, kwa sababu tumekamilisha shughuli za kikao hiki cha Seneti, ni wakati wa kuahirisha kikao hiki.

Kikao hiki cha Seneti kimeahirishwa hadi Jumanne, tarehe 9 Februari, 2021, saa nane unusu.

The Senate rose at 8.23 p.m.